

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA KUMI NA NNE

KIKAO CHA TATU

01 FEBRUARI, 2024



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA KUMI NA NNE

KIKAO CHA TATU – TAREHE 01 FEBRUARI, 2024

I. DUA:

II. MASWALI KWA WAZIRI MKUU:

III. MASWALI YA KAWAIDA:

OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

39. MHESHIMIWA TWAHA ALLY MPEMBENWE (KIBITI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itaanza ukarabati wa Shule chakavu za Msingi katika Jimbo la Kibiti.

40. MHESHIMIWA ZUBERI MOHAMEDI KUCHAUKA (LIWALE):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itaingia ubia na Wakala wa Nyumba Tanzania (TBA) kuwajengea nyumba Walimu nchini na kisha kuwakata kwenye mishahara yao.

41. MHESHIMIWA NASHON WILLIAM BIDYANGUZE (KIGOMA KUSINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itakamilisha ahadi ya Shilingi Milioni 10 za ujenzi wa Kituo cha Afya cha Kazuramimba.

OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO NA MAZINGIRA):

42. MHESHIMIWA SIMAI HASSAN SADIKI (NUNGWI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira):-

Je, sababu zipi zinasababisha eneo linaloathiriwa na Mabadiliko ya Tabianchi kupewa kipaumbele cha utekelezaji wa Mradi ili kunusuru hali hiyo.

WIZARA YA MAJI:

43. MHESHIMIWA JOSEPHINE JOHNSON GENZABUKE (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, lini Halmashauri ya Mji wa Kasulu itaondokana na matumizi ya maji machafu kutokana na ukosefu wa chujio.

WIZARA YA MADINI:

44. MHESHIMIWA IDDI KASSIM IDDI (MSALALA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Madini:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kufuta Leseni za Madini ambazo hazifanyiwi kazi na kuwapa Wachimbaji Wadogo.

WIZARA YA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:

45. MHESHIMIWA RASHID ABDALLAH SHANGAZI (MLALO):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuanzisha Somo la Uchambuzi wa Michezo katika Chuo cha Michezo Mallya.

WIZARA YA MALIASILI NA UTALII:

46. MHESHIMIWA ATHUMAN ALMAS MAIGE (TABORA KASKAZINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuifanya Asali kuwa moja ya Mazao ya kimkakati.

WIZARA YA NISHATI:

47. MHESHIMIWA AIDA JOSEPH KHENANI (NKASI KASKAZINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kumaliza changamoto ya kukatika kwa umeme Wilaya ya Nkasi.

IV. MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI:

(Kusomwa Mara ya Pili, Kamati ya Bunge Zima na Kusomwa Mara ya Tatu)

Muswada wa Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani wa Mwaka 2023.

Muswada wa Sheria ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi wa Mwaka 2023.

Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria za Vyama vya Siasa wa Mwaka 2023 *(The Political Parties Affairs Laws (Amendment) Bill, 2023.*

(Majadiliano yanaendelea)

**DODOMA
01 FEBRUARI, 2024**

**N.J. MWIHAMBI, *ndc*
KATIBU WA BUNGE**